

Uchanganuzi wa Hali (1999)



The Partnership for Child Development (PCD) was established in 1992 to help co-ordinate global efforts to assess the developmental burden of ill health and poor nutrition at school age. It brings together a consortium of countries, donor organisations and centres of academic excellence to design and test strategies to improve the health and education of school-age children.

The Partnership has international agency support from UNDP, WHO, UNICEF, The World Bank and British DFID, and is sustained through support from participating governments, the Rockefeller, Edna McConnell Clark and James S McDonnell Foundations and the Wellcome Trust.

The Scientific Coordinating Centre for the Partnership is based at:

**The Wellcome Trust Centre for the Epidemiology of Infectious Disease, University of Oxford,
South Parks Road, Oxford, OX1 3FY, UK.**

Tel: +44 (0) 1865 271 290 Fax: +44 (0) 1865 281 245

Email: child.development@ceid.ox.ac.uk Web: <http://www.ceid.ox.ac.uk/child/>

Utangulizi

Lengo kuu la uchanganuzi ulioelezwa katika makala haya ni kuelekeza mpango na tathmini ya mipango ya Afya na Lishe iliyoko mashuleni. Uchanganuzi wa hali ya afya na lishe unaweza kuelezewa kwa kina na kwa njia iliyo rahisi na ya kueleweka, lakini njia muhimu zaidi ya kukabili hali hiyo ni ya gharama ndogo, uchunguzi wa haraka unatoa majibu muhimu ya awali, kwa ajili ya juhudi za makusudi za kuanzisha au kuimarisha mipango ya Lishe na Afya mashuleni. Njia hizi za kuikabili hali hiyo iliyoorodheshwa katika makala haya siyo toshelevu, kuna uwezekano wa kuwepo vyanzo halisi na aina mbalimbali za habari ambazo ni muhimu na maalum kwa nchi au hali fulani tu.

Uchanganuzi wa hali ya Lishe na Afya unaofuata njia za kuikabili hali hiyo zilizoorodheshwa hapa unakusanya taarifa toshelevu kwa ripoti:

- Inayotambulisha matatizo ya afya na lishe kwa watoto wenye umri wa kwenda shule yanayostahili kupewa umuhimu wa kwanza;
- Hupima ushirikishwaji wa shule (viwango vya uandikishaji shule, kukaririsha darasa, na kuacha kabisa shule) na huelezea sababu kuu za utoro shuleni;
- Huelezea njia mbalimbali zilizo rahisi na za kudumu ambazo zinaweza kuboresha afya na lishe, mahudhurio na taaluma kwa watoto;
- Huelezea mapungufu makuu na matatizo yanayozikabili huduma za afya na lishe zilizomo mashuleni, na kutoa maoni juu ya njia zinazofaa za kurekebisha hali hiyo;
- Huelezea au hufahamisha juhudi za kusimamia na kutathmini huduma za lishe na afya mashuleni;
- Huelezea mambo muhimu yanayohitaji uchunguzi zaidi;

Taratibu za ukusanyaji taarifa hutoa pia fursa ya kuanzisha ushirikiano kati ya shule na maofisa wa afya, watoto wenye umri wa kwenda shule na vikundi vingine muhimu na mashirika mbalimbali. Uhusiano kama huo ni msaada mkubwa kabisa kwa mipango inayoinua huduma za afya na lishe mashuleni. Taarifa kuhusu uchanganuzi wa hali ya afya na lishe shuleni inaweza kupatikana kutokana na ukaguzi wa taarifa zilizopo, mahojiano na watoa habari wakuu, majadiliano ya vikundi vilengwa pamoja na mbinu nyingine za ukaguzi. Ukusanyaji taarifa umejadiliwa hapo chini kuhusiana na mambo muhimu, hata hivyo katika utekelezaji, kila ukaguzi, mahojiano au majadiliano hufuata (au huangalia) mambo haya kwa pamoja.

Ukaguzi zaidi wa kitaalamu utahitajika kabla ya mpango mpya wote kujitokeza kutokana na ripoti ya awali ya ukaguzi. Katika hali halisi uwekaji malengo ya njia za kurekebisha hali iliyopo bila shaka utahitaji changanuzi maalum zaidi pamoja na uchunguzi unaohusu taaluma ya tiba. Katika hali ya kuunga mkono uchanganuzi wote wa hali iliyopo ulioandikwa, ni lazima uchanganuzi huo ueleeze taarifa yake katika njia ya kuvutia na inayoweza kupatikana, na kutumia takwimu za aina mbalimbali ili kutoa msisitizo pamoja na taarifa ya kina. Kwa mfano, ulinganifu kati ya mapato ya kaya yanayotumika katika uvutaji na pombe na kiasi cha mapato yanayotumika katika huduma za afya ya watoto wenye umri wa kwenda shule, unaweza kuongeza mguso kutokana na picha halisi iliyoelezwa katika taarifa.

Kuainisha matatizo muhimu zaidi ya afya na lishe

TAARIFA INAYOHITAJIKA

Sababu za maradhi na vifo

Taarifa juu ya sababu za vifo na maradhi ni ya msingi katika uchaguzi wa njia muhimu za kurekebisha hali. Ni lazima takwimu zihusishe matatizo ya afya ambayo huanzia katika kipindi cha utoto na ujana lakini pia yanayoweza kujirudia yenyewe baadaye katika maisha- Virusi viletavyo upungufu wa kinga mwilini, kwa mfano. Licha ya sababu za ugonjwa na kifo, ni lazima taarifa ijumuishe umri na jinsia ya wale wanaohusika katika uchanganuzi, makazi yao na sehemu watokayo (kwa mfano, kama ni mjini au kijijini, sehemu zenye majimaji au kame) na kipindi cha hali ya hewa ambapo waliugua. Njia za kurekebisha hali zinazopangwa kutokana na matokeo ya uchanganuzi wa hali zinaweza basi kubainishwa kwa makini. katika hali halisi, mengi ya maelezo haya yanaweza yasipatikane, lakini ni muhimu kuelezea picha halisi ya hali iliyopo kadri iwezekanavyo.

Mwelekeo wa vifo na maradhi

Taarifa endapo kama tatizo la afya au lishe linaongezeka au kupungua kwa kipindi fulani, husaidia katika kubainisha mambo muhimu ya baadaye.

Kiwango cha njaa ya muda mfupi na utapiamlo

Ni lazima uchanganuzi utilie maanani matatizo ya lishe na njaa ambayo yanaweza yasijitokeze katika takwimu za afya.

Mabadiliko katika mpangilio wa tabia zihusianazo na afya

Ni vema uchanganuzi uamue jinsi gani mabadiliko katika tabia zinazohatarisha afya, kama vile madawa ya kulevya, uvutaji, kujamiiana katika umri mdogo na kujamiiana kusiko salama huathiri visababisho vya matokeo fulani, kama vile ya viwango vya ugomvi, mimba zisizotakiwa na utoro shuleni.

Mambo mengine yanayofifisha maendeleo ya taaluma shuleni

Ni muhimu uchanganuzi ukusanye taarifa juu ya kiasi cha matatizo yatokanayo na milango ya fahamu (athari za uziwi na upofu) na ulemavu mwingine wote kwa watoto wenye umri wa kwenda shule.

Nafasi ya visababisho vya matokeo vya kijamii na kiutamaduni kama vigezo vya afya

Uhusiano kati ya matatizo ya afya na lishe yaliyoainishwa kwenye tabia na tamaduni za jamii ni muhimu kwa mpangilio wa mpango na hasa kuhusiana na afya za watoto wa kike.

KUELEZEA TAARIFA

Ripoti na uchunguzi wa hali katika vitabu vya kimataifa na kitaifa

Vikundi vya Kisayansi (kwa mfano ofisi za Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto -UNICEF- na Shirika la Afya Duniani - WHO zilizopo katika kila nchi mwanachama, na Benki ya Dunia- (World Bank) vinaweza kufanya mapitio ya vitabu vya Kimataifa wakati taasisi wenyeji za utafiti zinajikita zaidi kwenye vitabu vya kitaifa. Vyanzo mbalimbali vya upatikanaji taarifa nje ya sekta za elimu na afya vinaweza vikawa vya manufaa, kwa mfano, kuchunguza makosa ya jinai kunaweza kukatoa taarifa muhimu kuhusu mpangilio wa tabia za vijana. Taarifa inatakiwa hasa kuhusu:

- Kifo na sababu yake;

- Upungufu wa virutubisho (kama vile Vitamini A, madini ya chuma na madini ya chumvi) vipimo vya urefu (urefu-kwa-umri, na uzito-kwa-urefu), njaa ya muda mfupi na vipimo vingine vya kiwango cha lishe;
- Maambukizo ya vijidudu, ukiwemo uambukizo wa malaria na minyoo;
- Mimba za utotoni na afya ya uzazi (magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya kujamiiana, UKIMWI, uambukizo wa njia ya uzazi, afya katika kipindi cha hedhi);
- Maambukizo ya njia za kupitishia hewa, ukiwemo ule wa kifua kikuu na homa za vipindi zikiwemo zile zitokanazo na ugonjwa wa malaria na maambukizo makali ya njia ya kupitishia hewa;
- Magonjwa yanayoweza kuzuilika (ugonjwa wa kupooza, pepopunda na homa ya matumbo);
- Uziwi na upofu, maambukizo ya ugonjwa wa ngozi na matatizo ya meno;
- Ulemavu sugu na magonjwa ya akili;
- Unyanyasaji wa kijinsia, ugomvi, ajali na uzoefu wa ulevi, tumbaku na madawa ya kulevya (vidonge).

Takwimu za mara kwa mara zihusuzo vifo na magonjwa kutoka vyanzo mbalimbali ndani ya nchi

Takwimu juu ya sababu za kulazwa wagonjwa na wale wanaohudhuria mahospitalini, kwenye kliniki na vituo vingine vya afya hutoa taarifa juu ya matumizi ya huduma hizo, lakini taarifa hizo huonyesha kupendelea eneo lililohusika pamoja na vikundi vya watu waliotumia huduma hizo za matibabu. Takwimu kutoka vituo vya afya vinavyopokea wagonjwa wa dharura zinaweza kuwa chanzo pekee cha taarifa zihusuzo ugomvi na ajali.

Mahojiano

Watoa taarifa muhimu ni pamoja na wafanyakazi katika Wizara ya Afya na ya Elimu, Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ambayo yanajihusisha na afya na vijana, vitivo muhimu vinavyohusika kutoka Vyuo Vikuu, wafanyakazi wa Afya pamoja na Maofisa kutoka sehemu inayohusika na makosa ya jinai. Uhojaji, unaofuata taratibu zilizoordheshwa hapo juu, utakuwa na lengo la kuhusisha sababu za afya mbaya na mipangilio ya afya ya taifa.

Dodoso na majadiliano kutoka katika vikundi vilengwa

Taarifa hizi zinaweza kutumiwa kuamua maoni ya walimu, wafanyakazi wa afya, wazazi na wanafunzi juu ya matatizo makubwa ya afya na lishe. Dodoso kama hizi pamoja na majadiliano zinaweza kuelezea vizuri zaidi kama kiwango cha kuelewa cha jamii juu ya chanzo na ueneaji wa matatizo ya afya hutofautiana na taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu. Ufahamu juu ya maoni hayo ni muhimu kwa ajili ya utayarishaji wa ujumbe sahihi katika elimu ya afya. Majadiliano yatawezesha pia kufanyika kwa uchunguzi juu ya athari zitokanazo na sababu za kijamii kama vile mgandamizo wa mawazo hasa katika tafsiri kama itakavyotumiwa na jamii kwa kigezo cha Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kuhusu uchanganuzi wa mazingira (kwa mfano, ukosefu wa ajira na mmomonyoko wa jamii). Dodoso pamoja na vikundi vilengwa vinaweza pia kutoa taarifa ya msingi juu ya aina za unyanyasaji kijinsia, taarifa ambayo inaweza kuelezewa vizuri kwa kutumia njia tofauti, na taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa kufuatana na vikundi kiumri, katika kuyakabili magonjwa yaenezwayo kwa njia ya kujamiiana.

Jinsi ya kutumia shule kikamilifu ili kufikia chenye umri wa kwenda shule

TAARIFA INAYOHITAJIKA

Ukubwa wa idadi kuu ya watoto wenye umri wa kwenda shule, uandikishwaji na viwango vya kuacha shule, pamoja na kiasi cha watoto wanaokariri madarasa

Taarifa hii huelezea mipangilio iliyoko katika vielezo vya sekta ya elimu. Ni lazima takwimu ijumuishe elimu ya msingi na ya sekondari pamoja na tofauti katika umri au madarasa, jinsia, mkoa na kiwango cha hali ya kimji.

Viwango vya utoro

Ni lazima uchanganuzi ukusanye taarifa- kwa majira ya mwaka, siku katika wiki kama nyongeza katika ile ya umri, jinsia, kiwango cha hali ya kimji na mkoa - juu ya watoto ambao waliorodheshwa katika shule lakini ambao hushindwa kuhudhuria mara kwa mara. Katika mikoa mingine, majira ya shughuli nyingi za kilimo, huwa na viwango vikubwa vya utoro hivyo itakuwa si wakati sahihi wa kutoa huduma za afya kupitia mipango ya afya shuleni. Vile vile utoro wa kiasi kikubwa wakati wa siku za soko (siku iliyowekwa maalum kwa ajili ya soko) utaonyeshwa na takwimu zinazohusu utoro wa siku katika wiki.

Sababu za kutokuandikishwa watoto pamoja na utoro

Sababu za msingi za utoro zinaweza zikawa miongoni mwa mambo muhimu makubwa ya kiafya, lakini kuainisha njia za kupunguza utoro ni muhimu kama watoto ni lazima wapatiwe elimu na njia za kurekebisha hali zilizopo kwenye mpango wa afya na lishe mashuleni.

Wajibu, unaowezekana kuwepo, wa elimu isiyo rasmi

Taarifa juu ya kiwango cha elimu isiyo rasmi inaweza kuelezea uwezekano wa kuwepo fursa zaidi za kutoa huduma za lishe na elimu ya afya pamoja na huduma nyinginezo. Sekta ya elimu isiyo rasmi inaweza kuwa ya manufaa kwa vikundi maalum kama vile wasichana au vijana ambao hawanufaiki na sekta ya elimu rasmi.

Sheria na sera sahihi kwa watoto wenye umri wa kwenda shule

Ni lazima taarifa ijumuishe sheria kuhusu kubughudhiwa kijinsiaunaofanywa na walimu, sheria inayokataza matumizi ya tumbaku na pombe, na sera juu ya kuruhusu wasichana wanaosoma na wakapata ujauzito, kurudi tena shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Gharama zitolewazo na jumuiya kwenye elimu, lishe na afya ya watoto wenye umri wa kwenda shule

Taarifa hii itaonyesha jinsi gani mipango ya lishe na afya shuleni inaweza kudumu kupitia michango pamoja na mikakati mingine itakayowekwa na jumuiya hiyo, juu ya upunguzaji wa gharama.

KUELEZEA TAARIFA:

Ripoti na uchunguzi ndani ya vitabu vya Kimataifa na vya Kitaifa

Vitabu vilivyoandikwa kitaifa, hasa kutoka katika Wizara ya Elimu, vinaelekea kuwa vya manufaa zaidi.

Taarifa zilizokusanywa na huduma za elimu kutoka mkoani na wilayani

Nyingi ya taarifa zilizokusanywa zimetokana na mihtasari iliyopatikana kutoka vituo tofauti tofauti katika sehemu mbalimbali, lakini uchanganuzi wa taarifa hizo unaweza kuhitaji utaalamu maalum kama ule unaopatikana katika taasisi za utafiti za elimu.

Mahojiano

Tazama sehemu hii hapo juu.

Kushirikiana taarifa zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali

Mihtasari ya takwimu zilizokusanywa zinaweza kutumika pia na walimu, wafanyakazi wengine katika sekta za afya na elimu, na wanafunzi wakubwa ambao wanaweza kutoa maoni kama takwimu zinazoonyesha sababu muhimu za uandikishaji watoto shule na utoro. Juhudi za makusudi zitahitajika kuwahoji vijana wadogo ambao hawajaandikishwa shule, au ambao ni watoro wa mara kwa mara, pamoja na wazazi wao. Mahojiano kama hayo yanaweza kutoa taarifa juu ya utekelezwaji wa sheria na sera pamoja na jinsi gani vyombo kama hivi vinatafsiriwa.

Kutathmini uwezo wa kuboresha na kutekeleza mipango

TAARIFA INAYOHITAJIKA:

Huduma za lishe na afya kwa watoto wenye umri wa kwenda shule zilizopo

Jambo la kufikiriwa kwanza, siyo tu mipango ya shule iliyopo, bali pia huduma za afya kwa ujumla ambazo zimelengwa kwa watoto wenye umri wa kwenda shule. Taarifa juu ya upatikanaji wa vifaa na njia kuu za kupatia fedha zitakuwa muhimu katika kuchunguza uwezo wa sehemu fulani pamoja na mwitikio wa watu wa sehemu hiyo. Mada za msingi zinahusu:

- Majukumu maalum juu ya sekta za afya na elimu kwa lishe shuleni na elimu ya afya pamoja pia na huduma nyinginezo;
- Sera za kitaifa na za kimkoa zinazohusiana na lishe na mipango ya afya mashuleni - umuhimu wake na ni kwa kiasi gani mipango hiyo inaruhusu marekebisho;
- Muundo, sehemu mbalimbali za muundo huo, na ukamilishwaji wa mipango ya lishe na afya mashuleni, ikihusisha pia uchunguzi wa kawaida wa afya na mipango ya huduma ya kwanza;
- Njia za kerekebisha hali ya utoaji elimu ya afya zilizopo, zikihusu pia hali ya maisha ya familia na elimu ya uzazi bora, na shughuli nyingine zinazohusu lishe na afya, kwa mfano vyama vya afya mashuleni;
- Matumizi ya huduma za afya ya msingi zinazotumiwa na kundi lenye umri wa kwenda shule, ukihusisha matumizi ya huduma za afya ya uzazi za rufaa zinazofanyika kati ya shule na mfumo wa usimamizi wa afya ya msingi;
- Kiwango ambacho watoto wenye umri wa kwenda shule hutumia huduma za afya za watu binafsi pamoja na huduma za waganga wa jadi;
- Maudhui, ukamilishwaji, ubora na gharama za mipango ya chakula shuleni na bustani zilizo shuleni;
- Taarifa juu ya migahawa iliyopo shuleni na chakula kiletwacho na watu walioko karibu na shule, wanaolisha mashule;
- Taarifa juu ya upatikanaji wa maji shuleni na vyoo, na huduma za kuondoa maji machafu;
- Mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na mashirika yanayoshirikisha serikali mbalimbali, kwa mipango ya shule;
- Mchango wa jumuiya kwa shule na afya, ikihusu pia utoaji wa maji safi na huduma nzuri za vyoo, chakula mashuleni na huduma nyinginezo za lishe na afya;
- Viwango vilivyopo vya uwekezaji katika afya na lishe kwa watoto wenye umri wa kwenda shule, unaofanywa na serikali au mashirika mengine;
- Utoaji wa elimu ya awali na elimu maalum.

Mipango juu ya uendelezaji huduma kwa watoto wenye umri wa kwenda shule

Ni muhimu kupanga upatikanaji wa vitendea kazi na uwezo wa kitaalamu na ki-taasisi kwa ajili ya kuendeleza huduma kwa kutumia:

- Mahojiano ya watu muhimu na taasisi zenye wataalamu wanaotahili na zenye kuonyesha mwamko;
- Uchunguzi wa uwezo na udhaifu wa wakala wakuu na mashirika mengine yanayoshiriki katika mipango ya lishe na afya shuleni.

Uwezo wa sekta ya elimu katika kusaidia kutoa huduma za lishe, elimu ya afya na huduma nyinginezo

Msisitizo juu ya takwimu za gharama utasaidia katika uchunguzi wa kuendesha na kudumisha mpango wa lishe na afya. Taarifa inayohitajika:

- Idadi na usambazaji wa shule za msingi na sekondari na walimu, vikiunganishwa na idadi ya wafanyakazi katika kliniki na wafanyakazi wa afya;
- Maudhui kuhusu lishe na elimu ya afya yafundishwayo mashuleni, ikujumuisha malengo, njia za ufundishaji, vifaa na maoni juu ya muhtasari unaotumika au unaofanyiwa majaribio;
- Uwezo wa vyyo vya Ualimu wa kutoa mafunzo juu ya lishe na afya, ikijumuisha pia kiasi cha mafunzo yatolewayo kwa walimu walio kazini;
- Mchango wa vikundi vya dini na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali (NGOs) katika sekta ya elimu na uwezo wa mashirika kama hayo katika kusaidia utoaji wa lishe, elimu ya afya na huduma nyinginezo;
- Utayari na uwezo wa mazingira ya shule kusaidia kuboresha afya, pamoja na upatikanaji wa maji safi na huduma muhimu kwa wasichana walio vunja ungo waliopo shuleni.

Changanuzi za hali ya sekta za elimu na afya zifanywazo na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) zinaweza kuwa na taarifa juu ya baadhi ya mambo haya au changanuzi hizo zinaweza kutoa msingi wa kufanyia ulinganifu. Kwa mfano, ulinganifu mmoja wa taarifa unaweza kuwa kati ya aina ya maji na huduma za kuondoa maji machafu shuleni, na kati aina ya maji na huduma za kuondoa maji machafu majumbani na kwa jamii nzima.

Upatikanaji wa vitendea kazi

Vitendea kazi muhimu vitatoka katika sekta mbalimbali ambazo ni muhimu kwa afya na elimu (za kiserikali, zisizo za kiserikali, na sekta baina ya serikali mbalimbali) na hata kutoka kwa watoto wenyewe na jamii kwa ujumla. Taarifa pia ni muhimu juu ya gharama za fedha na matumizi ya njia za kurekebisha hali zilizopendekezwa.

Upatikanaji wa vitendea kazi kutoka katika sehemu maalum

Sehemu maalum zinaweza zikawa vilabu vya michezo na mashirika ya dini, vikundi vya shughuli za kijamii na vyombo vya habari. Michango kutoka katika vyanzo kama hivi inaweza kuwa muhimu hasa katika kudumisha uhai wa mipango ya afya na lishe shuleni.

KUELEZEA TAARIFA

Taarifa nyingi muhimu zitakuwa zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali katika chunguzi za vitendea kazi vilivyopo pamoja na uwezo uliopo. Vyanzo vya ziada vimeelezwa kwa kina zaidi katika vipengele vinavyohusika hapo juu.

Further information and references

CONTACT DETAILS

Partnership for Child Development (PCD)
 Scientific Co-ordinating Centre
 Wellcome Trust Centre for the Epidemiology of Infectious Disease
 Zoology

Department of
 South Parks Road
 Oxford
 OX1

3FY
 UK
 Tel: +44 1865 271 290
 Fax: +44 1865 281 246
 Email: child.development@ceid.ox.ac.uk
 Web: <http://www.ceid.ox.ac.uk/child>

Bradford Strickland
 USAID Bureau for Africa
 Office of Sustainable Development Education Team
 Washington, DC 20523
 Tel: +001 703 235 4970
 Fax: +001 703 527 4661
 Email: bstrickland@usaid.gov

Organización Panamericana de la Salud (PAHO)
 Regional de la Organización Mundial de la Salud
 Third Street, N.W.

Oficina
 525 Twenty
 Washington, D.C. 20037
 USA

Bruce Dick
 Youth Health Promotion Unit, UNICEF
 UNICEF House
 3, UN Plaza
 New York, NY
 Tel: +001 212 303 7644
 Fax: +001 212 326 7336
 Email: bdick@unicef.org

David Evans
 Task Force on School Aged Children

WHO

CH-1211 Geneva 27
 Switzerland
 Tel: +41 22 791 3767/8
 Fax: +41 22 791 4181

International School Health Initiative at the World Bank (ISHI)
World Bank
1818 H Street, N.W.
Washington, DC 20433
USA
Tel: (202) 458 5000
Email: eservice@worldbank.org

The

SELECTED USEFUL REFERENCES

- Bundy, D.A.P. & Guyatt, H. (1996) Schools for Health: Focus on health, education and the school-age child. *Parasitology Today* 12 :1-16
- Del Rosso, J. & Marek, T. (1996) Class Action: Improving School performance in the Developing World through better Health and Nutrition. Directions in Development. World Bank, Washington, DC.
- Hall, A. & Bundy, D.A.P. (1998) The Partnership for Child Development: promoting the health, nutrition and education of school-age children *Sub-Committee on Nutrition (SCN) News* 16, July 1998
- Hall, A., Adjei, S. & Kihamia, C. (1996) School Health Programmes. *Africa Health* 16 (6) 22-3
- Meresman, S. (1998) The Ten who go to School. School Health and Nutrition Programming in Latin America and the Caribbean. World Bank/PAHO, Washington, DC.
- PAHO/WHO (1996) Escuelas Promotoras de Salud: Modelo y Guía para la Acción. Serie HSP/SILOS #36, OPS, Washington, DC.
- PAHO/WHO/CDC (1997) Identificación y Vigilancia de Practicas de Riesgo con Escolares y Adolescentes. HPP/HPL, OPS, Washington, DC
- Puertas, E.B. & Cerqueira, M.T. (1996) Análisis Descriptivo de la Situación the la Salud Escolar en Varios Países de la Región. HPP/HPL, OPS, Washington, DC.
- The Partnership for Child Development (1997) Better Health, Education and Nutrition for the School-Age Child. *Transactions of the Royal Society of Tropical Medicine and Hygiene* 91: 1-2
- The Partnership for Child Development (1998a) The Anthropometric status of School Children in five countries in the Partnership for Child Development. *Proceedings of the Nutrition Society* 57:149-158,
- The Partnership for Child Development (1998b) The Health and Nutritional Status of School Children in Africa: evidence from school-based health programmes in Ghana and Tanzania. *Transactions of the Royal Society of Tropical Medicine and Hygiene* 92:254-261
- UNICEF 'Tools for Situation Analysis – Adolescent Health' *waiting for details*
- WHO (1998) Guidelines for the evaluation of soil-transmitted helminthiasis and schistosomiasis at community level: A guide for managers of control programmes WHO/CTD/SIP/98.1: WHO Geneva
- WHO (1998) WHO's Global School Health Initiative. Health Promoting Schools. A healthy setting for living, learning and working. WHO/HPR/HEP/98.4. WHO, Geneva.